



Wema ni tabia njema, na dhambi ni lile litakalokukereketa katika kifua chako, na ukachukia watu wasilione

Kutoka kwa Nawwasi bin Samaan Al-Answari radhi za Allah ziwe juu yake amesema:
Nilimuuliza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu wema na dhambi, akasema:
"Wema ni tabia njema, na dhambi ni lile litakalokukereketa katika kifua chako, na
ukachukia watu wasilione".

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Aliulizwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu wema na dhambi, akasema: Kubwa kabisa katika wema ni tabia njema pamoja na Allah, kwa kumcha, na pamoja na watu, kwa kuvumilia kero, na kupunguza hasira, na kukunjua uso, na kuwa na maneno mazuri, na kuunga udugu na kutii na kuwa mpole na kutenda wema, na kuishi vizuri na familia, na kusuhubiana na watu vizuri. Na ama dhambi ni kila kitakachokereketa ndani ya nafsi katika mambo yenye kutatiza, na kifua kikakosa utulivu na kutokunjuka, na moyo ukapata shaka, na ukaogoga kwa sababu ni dhambi, na ukawa hukutaka kulidhihirisha kwa mtu au hadharani mbele za watu kwakuwa ni baya, na hii ni kwa sababu nafsi hupenda watu waone yale mazuri yake, ikiwa itachukia watu kuyaona baadhi matendo yake basi hayo ndiyo madhambi wala hayana kheri ndani yake.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4308>

